


# K.O.K.W.A

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

***Mmoja alikuwa mtu mzima sana kiasi kwamba hata ngozi yake ya uso ilikwishaanza kuwa na makunyanzi na mwingine alikuwa kijana aliyevaa kama askari binafsi, nguo nyeusi na mikono yake ilifunikwa kwa glavu nyeusi. Pembeni yao kulikuwa na gari kubwa la kisasa, Toyota Land Cruiser. Hili lilikuwa ni moja ya magari hadimu kuonekana katika Madagaska. Wale wanajeshi na mzigo wao na yule mwanamke aliyejitambulisha kwa jina la Afrika akiwa bado katika usingizi mzito walipanda kwenye lile gari pamoja na wenyeji wao. Safari kuelekea pasipojulikana ikaanza.***

## SEHEMU YA 06

✠ ✠ ✠

Kamanda Amata aliegesha gari nje ya jengo la Makumbusho ya Taifa saa tano asubuhi siku iliyofuata. Nje ya jengo hilo katika Mtaa wa Shaaban Robert shughuli zilikuwa zikiendelea kama kawaida. Akatazama harakaharaka huku na huko, na kwa sekunde hizo chache alizotazama alikwishaona vitu na mambo mengi ambayo ingekuwa wewe usingeyaona. Akavuta hatua na kuzikwe ngazi mpaka mapokezi. Katika dawati la mapokezi, alipokelewa na kijana mtanashati aliyevalia kitamaduni na kupendeza kwelikweli. “Naweza kumwona mkurugenzi Bwana Kisinini?” akamuuliza mara baada ya kumsabahi.

“Aaaan siamuona kufika leo, ila jana niliskia kuwa atakuwa na kikao wizarani kule Dodoma… lakini ngoja tujiridhishe,” yule

kijana akajibu na kuinua simu iliyokuwa mezani. Akapiga upande wa pili, na simu ile ikapokelewa na mwanadada. Amata alilijua hilo maana aliisikia sauti hiyo kwa mbali. Mara baada ya kumaliza kuongea na simu ile, aliirudisha kwenye kifarasi chake. "Katibu wake anasema hajafika, na kuhusu kikao ni kesho huko Dodoma…" yule kijana kamweleza Amata.

"Kwahiyo aliaga kama ndiyo anaenda Dodoma au la?" Amata akauliza.

"Hapo siwezi kujibu mheshimwa, labda nikuelekeze ofisini kwake, katibu wake atakupa maelezo yote!" yule kijana akamwambia Amata na kumchukua mpaka ghorofa ya pili.

Ndani ya ofisi hii palikuwa na sehemu mbili ambazo zilitengwa kwa kioo kizito na kuta za alumminium. Katika sehemu hii ya kwanza aliketi mwanadada mwenye mwili wa kutosha kwa kadiri ya kilo tisini mpaka mia moja na kumi hivi akiwa ndani ya suti safi ya kijivu na blauzi nyeupe iliyomkaa vyema. Yule kijana akamkabidhi kwa huyo mwanadada kisha yeye akaondoka zake.

"Mimi ni mgeni wa Bwana Kisinini, alinambia nifike hapa leo…" Amata akamwambia yule katibu. Mwanamke yule akashusha pumzi na kujiweka vizuri kitini.

"Mkurugenzi leo hajafika, name nashangaa mpaka sasa… siyo kawaida yake. Kwa sababu yeye hata akiwa na safari, asubuhi lazima afike ofisini halafu saa nne hivi huwa anaanza safari kutokea hapa," akasema. Amata akatulia kimya na kujaribu kuimeng'enya ile taarifa.

"Umempigia simu yake?" akauliza.

"Nimepiga mara tatu haijapokelewa, kwa sababu kuna makabrasha hapa ilimbidi kusaini kabla hajaondoka, sijui ana

shida gani," yule katibu akaeleza. Amata muda wote alikuwa akitazama lugha ya mwili ya mwanamke yule na kujiridhisha kuwa ni kweli hajui chochote kingine kuhusu bosi wake.

"Anaishi wapi?"

"Tegeta block A, namba 162," yule mwanadada akajibu, "Una shida ya kiofisi au binafsi?" akauliza.

"Ni binafsi, ila alinambia nije hapa… anyway, basi nitajaribu kumpigia. Asante kwaheri," Amata akaaga na kuondoka kwenye lile jengo. Alipofika nje na kuliendea gari lake, akashtuka kukuta limezuia na gari jingine ambalo liliegeshwa nyuma yake. *Huyu dereva kasoma shule au kajifunzia uwani?* Akajiuliza. Nyuma ya gari lake liliegeshwa Toyota Hilux Double Cabin jeusi. Ndani hakuweza kuona chochote kwa kuwa gari lile lilikuwa na vioo vyote vyeusi. Hakuhangaika kumtafuta mwenye hilo gari, tayari akili yake ilikuwa mbele zaidi. Akaondoka zake, mpaka upande wa pili wa lile jengo, akachukua barabara ya Sokoine mpaka karibu na ofisi za TBA, hapo akakuta gari lao jingine, akaliendea na kuingia. Akaketi nyuma ya usukani kimya. Dakika kumi zilimtosha, akawasha lile gari na kuliondoa taratibu, akasunguka kupitia Barabara ya Luthuli kisha akakunja na kurudi na ile ya Samora mpaka alipoikuta Barabara ya Shabaan Robert, akakunja kona kushoto na kupita tena mbele ya jengo la Makumbusho kwa mwendo wa taratibu. Mara hii hakulikuta lile Toyota Hilux na gari lake lilikuwa bado maegeshoni. Kwa mwendo uleule, aliendelea mbele na kuipita Barabara ya Sokoine, kisha akachukua Barabara ya Luthuli na kurud na ile ya Kivukoni mpaka jengo la Wizara ya Ardhi akaegesha gari hapo na kuteremka. Hatua zake zilikuwa ndogondogo kurudi Ofisi Ndogo. Alipopita mbele ya jengo lenye ofisi ndogo za Bunge

akatazama upande wa maegesho ya ndani pale ambapo siku iliyotangulia paliegeshwa lile gari lililomgonga Madam S. Alichokiona kilimvutia. Alimwona Nuru, mwanamke aliyemwambia Amata kuwa yeye ndiye mmiliki wa lile Mazda akiwa amesimama na kijsna mmoja mrefu na aliyejaa misuli ya mwili. Amata alilitambua hilo kutokana na fulana ya mpira aliyovaa kijana huyo. Kilichomshtua ni kuwaona wawili hao wakiwa kwenye hali ya ubishano huku wakilizunguka lile gari. Amata akatazama huku na huko, akavuka barabara mpaka kwa jamaa aliyekuwa akiuza madafu ambaye basikeli yake alikuwa kaiegemeza kwenye ukuta wa jengo la Wizara ya Elimu. Akiwa anaandaliwa dafu lake, alimwona Nuru akimkabidhi ki-shari funguo kijana huyo. Yule kijana aliingia garini na kuliwasha. Mlio wake mnene uliufanya moyo wa Kamanda kuona naam lilikuwa Sports Car. Yule jamaa akaligeuza na kulitoa nje ya geti ya ile ofisi. Nuru alionekana kuangalia tu na kisha kuondoka zake kurudi ofisini. Simu ya Amata ikatetema, akaitoa na kuifungua. Akakuta taarifa ya mtandao katika mfumo wa satelaiti ikimwashiria kuwa GPS imeanza kufanya kazi. Akatabasamu!

Akachukua dafu lake na kulifakamia, kishapo akavuta hatua kurudi Ofisi Ndogo. Hapo hakukaa, aliingia na kuchukua gari lililokuwa maegeshoni, akaondoka zake. Alipotazama mfumo wake wa GPS kwenye lile gari, aliliona lile Mazda likiimaliza barabara ya Ocean na kuikamata ile ya Bagamoyo. *Mimi na wewe mpaka mwisho!* Akawaza na kuondoa gari kuingia barabarani. Safari ya lile Mazda iliishia Kunduchi,Mtongani Beach Resort. Amata aliendesha gari taratibu akaipita ile resort na kusimama mbele kama mita mia mbili hivi. Alipoegesha vizuri, akashuka na kurudi kwa miguu mpaka kwenye ile resort. Hapakuwa na watu

wengi kwa sababu labda ilikuwa siku ya kazi. Lakini waliopo aliwatambua vizuri kuwa ni wageni waliokuja kupumzika au kupata huduma mbalimbali zinazopatikana hapo. Kamanda Amata akavuta hatua mpaka lilipo duka la vinywaji, lakini jicho lake lilikuwa makini kumtazama yule kijana kaelekea wapi. Baada ya kukamata bia yake ya kopo mkononi na pakiti ya korosho mkono mwingine. Alilizunguka lile eneo kwa kupita sehu moja mpaka nyingine. Ni kule upande wa baharini ndiko alikomuona yule jamaa akiwa kasimama na mtu mwingine. Hakuona sura zao kwa kuwa walikuwa wamempa mgongo. *Haina shida nitasubiri wageuke!* Akawaza na kutafuta eneo zuri la kuketi. Waswahili walisema 'Subira huvuta kheri', naam wale jamaa waligeuka na kuelekea upande ule aliokuwa ameketi Amata. Macho yake yakiwa ndani ya miwani maalum, aliweza kuwaona wawili wale wakitembea na kusimama huku wakiongea jambo fulani. Hapa, mara moja, alimtambua Braison Sambala. Kijana mtanashati, aliyevalia shati safi jeupe na suruali ya dengiriz yaani jinzi. Miwani ya Amata ilikuwa ikichuku picha mnato kwa ukimya wa hali ya juu. Usingejua kama inafanya hivyo kwa kuwa kazi ya Amata ilikuwa ni kutikisa kichwa kidogo halafu yenyewe ingechuku picha sekunde mbili baadae. Wawili wale walipotokomea, Amata aliinuka kutoka pale alipokeati na kuzunguka upande mwingine tofauti na ule waliopita. Akawaona wamesimama nje ya lile Mazda, mazungumzo yakiendelea. Baada ya dakika kama tatu hivi walipeana mikono na kuagana. Lile Mazda liliondoka na yleyule kijana na Braison alirudi katika ile Resort, safari hii alikwea ngazi na kupandisha ghorofa ya kwanza. Amata aliweza kumuona vyema kwakuwa korido za jengo lile zilikuwa kwa nje, wazi. Alimuona mlango aliouingia na

kujifungia. “Nitakurudia baadaye!” akajisemea na kisha kulirudia gari lake.

✠ ✠ ✠

Alipoketi tu kitini, nyuma ya usukani na kuwasha gari, redio iliendelea na taarifa za mchana huo.

*‘…mashuhuda wa tukio hilo wanasema kuwa,*
*Bwana Kisinini amekutwa ndani ya gari lake*
*akiwa hana uhai asubuhi ya leo.’*

*Kisinini huyuhuyu?* Akajiuliza. Amata akainua simu yake na kubofya namba kadhaa kisha akaiweka sikioni.

“Nimesikia habari ya kutatanisha hapa rediona saa saba hii…” akamwambia mtu wa pili.

*“Nini tena?”* Inspekta Simbeye aliyekuwa upande wa pili akauliza.

“Kisinini amekutwa amekufa ndani ya gari lake…”

*“Mh!”* akashangaa. *“Ngoja nilifanyie kazi nitakwambia,”* Inspekta Simbeye akamaliza na simu ile ikakatwa.

Kamanda Amata akaiacha barabara ya Kunduchi na kukamata ile ya Bagamoyo kuelekea Tegeta. Akilini mwake, sasa alikuwa na jambo moja tu, kufika nyumbani kwa Bwana Geofrey Kisinini. Alikumbuka maelekezo kutoka kwa katibu muhtasi wake. *Tegeta Block A 162!* Alikumbuka.

## Tegeta Block A, 162

Kamanda Amata aliegesha gari nje ya nyumba ile, umbali wa mita takribai hamsini kutoka nyumbani hapo. Hapakuwa na watu wengi lakini ingia-toka za kimsiba zilionekana tangu nje. Kwa hatua za haraka haraka aliifikia nyumba ile. Geti lilikuwa wazi kama ihsra kwamba kila mtu aingine. Ndani ya nyumba vilio vilisikika hasa vya kina mama na huku nje vikundi vikundi vya akina baba vilisimama hapa na pale. Amata akatazama kila upande na kumwendea mmoja wa vijana aliyekuwa amekati peke yake. Akamsabahi.

"Samahani ndugu, nani amekufa hapa?" akauliza kwa sauti ya upole na sura iliyojaa majonzi.

"Ah Dingi mdogo, mwenye nyumba hii…" yule kijana alijibu huku akijifuta machozi.

"Oh pole sana!" Amata akampa pole huku akimpigapiga begani, "Ilikuwaje, ugonjwa au nini?" akauliza.

"Hapana braza, heri ingekuwa ugonjwa… inasemekana alitoka hapa asubuhi na rafiki yake kuelekea mjini. Ila yeye dingi mdogo alikuwa na safari ya Dodoma kikazi. Lakini mwili umegunduliwa hapo Tangi Bovu, gari likiwa nje ya barabara limeegeshwa," akaeleza. *Huyo rafiki yake ndo atakuwa amemuua?* Akajiuliza.

"Huyo rafiki yake mnamjua?" akahoji.

"Mimi binafsi simjui, ila wanasema ni mzungu, ana nywele nyeupe hivi… alikuja hapa mapema asubuhi, wakanywa chai pamoja na kuanza hiyo safari…" yule kijana akaeleza wazi. *Rafiki, mzungu!* Amata akawaza. Alipomaliza kuzungumza na yule kijana akatoka mpaka eneo jingine palipokuwa na kikundi cha watu japo kusikia kinachozungumzwa. Hapakuwa na jipya zaidi ilikuwa ni mipango ya wapi wakaazime maturubai. Akatoka nje ya geti

huku akijifanya kuongea kwa simu na kurudi mpaka kulifikia gari lake. *Rafiki, Mzungu, je anaweza kuwa ndiyo muuaji? Huyu mzungu mbona hakuwapo garini, au alishuka kabla Kisinini hajauawa, au alimuua kisha ndo akashuka?* Maswali mengi yalikuwa yakikizunguka kichwa cha Amata. Damu yake ilimchemka kwelikweli. Sasa alishaanza kuona tangu sakata la Madam S anaanza kukutana na mengine. *Ajali ya Madam S ina uhusiano na upotevu wa Kokwa? Maana hapa naona kifo cha Kisinini kina mahusiano kwa ailimia karibu sabini na tano na upotevu wa Kokwa. Kisinini hakutakiwa kutoa ushahidi wowote hivyo ilikuwa lazima wamzimishe. Baaas… huyu Mzungu ndiye kamuua Kisinini… sasa je; huyu Mzungu ni nani?* Akajiuliza huku akichakata mawazo ilia pate taswira nzuri ya matukio hayo.

Taarifa za kifo cha Geofrey Kisinini zilisika mezani pa Madam S. naye hakuwa na hoja nyingine zaidi ya kumwambia Amata aendelee kufuatilia ili ajue ukweli lakini aingine kwa kina zaidi katika hilo ili kuzuia kama kuna viashiri vyovyote vya hatari kwa wengine. Akaitwaa simu yake na kuiweka sikioni mara baada ya kumaliza kubofya namba za huyo aliyekuwa akimtaka. Hakuwa mwingine bali Inspekta Simbeye.

"Aaaah langu moja tum zee," akasema Amata.

*"Mhhh! Mhhhh… niambie…"* Inspekta akasema kutoka upande wa pili.

"Vipi umeshauona mwili wa Kisinini?" Amata akahoji.

*"Hapana mi siye daktari …"* Inspekta akajibu. Kamanda Amata alielewa maana ya jibu hilo na kule kujikohoza kwa mwanzo. Kwake ilikuwa na maana kuwa alipo Inspekta Simbeye hapafai kuzungumza suala nyeti kama hilo.

“Hospitali gani nzuri?” Amata akauliza lakini alikuwa akiimanisha kuwa mwili upo hospitali gani.

*“Kwa ugonjwa wako fika Mwananyamala, muone mtu anaitwa Kassim Malimbichi, mwambie wewe ni mtoto wa Simbeye!”* baada ya maneno hayo, ile simu ikakatwa. Anakaje simu huyu kwani yeye ndiye kapiga? Amata akajiuliza. Siku zote, aliyepiga simu ndiye anayetakiwa kukata simu. Hiyo ni itifaki ya kimataifa katika uga wa mawasiliano ulimwenguni.

✠ ✠ ✠

Daktari Kasimu Malimbichi alikuwa akivua glavu zake na kuzitia kwenye pipa la taka aliposikia hodi ikibishwa katika chumba alichokuwamo. Kabla hajaitikia hodi ile, akavua koti na kulitundika pahala pake. Hodi iliendelea kubishwa wakati naye akiufikia mlango na kuufungua. Macho yake yakagongana nay ale ya Kamanda Amata.

“Karibu nikusaidie, ila kama una shida binafsi basi ukanisubiri ofisini,” Kasimu akamwambia Amata.

“Nimeagizwa na Inspekta Simbeye kwako…” Amata akasema.

“Oooh kijana wa Simbeye…” Kasimu akatamka huku akitabasamu na kumpa ishara ya kuwa aingie ndani, “Nitakukaribisha hapa japo siyo pazuri sana,” akamwambia Amata.

“Usihofu daktari… kanambia niulize swali moja tu…” Amata akapunguza sauti.

“Enhe!” Kasimu akajibu kwa kutaka kusikia hilo swali huku mikono yake akiishikamanisha viganja na kuiweka juu ya meza.

“Mmeshafanya uchunguzi wa mwili wa Kisinini?”

“Tayari… mwili haukuhitaji uchunguzi nkubwa maana marehemu kavunjwa shingo. So kifo chake ni kunyongwa kwa mkono na kuvunjwa mifupa ya shingo,” yule daktari akatoa mpaka jibu ambalo hakuulizwa.

Amata akanyamaza kimya kwa jozi la sekunde, kisha akamtazama daktari, “Hakuna jingine mmeona?”

“Hakuna labda kama polisi wana taarifa nyingine maana daima kuna maeneo hatuingiliani, sisi madaktari tunachunguza zaidi sababu za kifo cha mtu kitabibu, mfano kauawa kwa sumu, aku kapigwa maana yake ana majeraha, au kama hivi kanyongwa… unaona ee! Ila polisi wao wanachunguza zile alama za vidole, mwonekano wa marehemu mwenyewe kama kafa anatabasamu au anahusunika…” daktari Kasimu aliposema hayo Amata akaangua kicheko.

“Nashukuru daktari, basi ngoja nimfikishie taarifa mzee…”

“Haina tabu kijana karibu tena!”

Daktari Kasimu alikuwa na umri unaorandana na Inspekta Simbeye kwa muonekano. Amata aliondoka zake na kumwacha yule daktari akiendelea na shughuli nyinginezo. Mwendo wake wa gari ulikuwa si mkubwa sana wala mdogo sana, aliendesha huku kichwa chake kikiwa kimejawa na mawazo lukuki. *Mzungu kamnyonga Kisinini kwanini? Na Mzungu huyu ni nani?* Akajiuliza. Amata akaegesha gari lake maeneo ya Faya na kuteremka. Akavuta hatua mpaka katika ukuta wa kituo cha Zimamoto jirani na kona ya kuelekea Muhimbili. Hapo palikuwa na kioski kidogo cha vinywaji. Akaagiza koka baridi na kuketi kwenye kiti upande wa nje. Akachukua simu yake na kumwandikia ujumbe Inspekta Simbeye.

*'Naomba upelelezi ufanyike kuhusu maisha ya Simbeye,*
*Ikiwamo marafiki zake na sehemu anazopenda kutembelea.*
*Pia kama ana nyumba ndogo zijulikane na biashara zake na kila kitu*
*Saa ishirini nan ne zitumike, kesho nitafata taarifa ofisini kwako muda*
*kama huu…'*

Kamanda Amata aliutuma ujumbe ule na kisha akafungua sehemu nyingine ya simu ileile na kutazama GPS yake inaonesha lile gari lipo wapi. Moyo wa Amata ulipiga kwa kishindo baada ya kuona GPS ikimwonesha kuwa lile gari liko maeneo ya Tegeta Block A. kengele za hatari kichwani mwa Amata zikalia. *Uwepo wa gari hili mahala hapa kunaashiria kuwa kuna uhusiano mkubwa wa ajali ya Madam S, Kuuawa kwa Kisinini na upotevu wa Kokwa… sawa nideal nao perpendicular!* Akawaza. Kwa hilo, hata ile soda haikuweza tena kushuka kooni. Akainuka. Akalipa. Akaondoka. Safari yake ilikuwa moja kwa moja mpaka ofisini kwake, JM Mall Mtaa wa Samora. Akaegesha gari na kuteremka. Kambarau ya jengo lile ikamfikisha ghorofa ya sita. Moja kwa moja mpaka AGI Invenstiment. Akasukuma mlango na kuingia. Gina alikuwa mezani pake ametingwa na kufuatilia habari mbalimbali za ulimwengu kupitia kompyuta yake.

Baada ya kusalimiana, moja kwa moja aliingia kwenye ofisi yake na kuketi kitini, akashusha pumzi ndefu na kujiegemeza kitini. Gina aliingia dakika hiyohiyo na kumkuta Amata kajiegemeza kitini huku macho yake yakiwa yamefumbwa.

"Vipi?" akamuuliza.

"Kuna kitendawili cha kutegua usiku huu… tukifanikiwa basi kazi ya kufanya itajulikana," Amata akasema huku bado akiwa kafumba macho yake.

"Kuhusu nini zaidi?"

"Yote tunayoyashughulikia nayaona yamejifunga katika fundo moja, sasa ili tuweze kulifungua na kujua kipi ni kipi, basi usiku wa leo ni muhimu sana," Amata akajibu. Alipofumbua macho yake, akajiweka vizuri kitini na kumtazama Gina aliyeketi kiti cha wageni. Msichana mzrembo wa Kingoni ambaye Mungu hakumnyima mwili mtamu bali alimjali kadiri ya alivyoona inafaa. Macho yake ya duara ndiyo kabisa yalikuwa yakiongea urembo wa sura yake. Na kwa ajinsi alivyokuwa akiijua sanaa ya kuweka nywele zake, alipendeza kwelikweli. Ukiachana na uhusiano wa kikazi kwa wawilio hao, Gina na Amata walikuwa na uhusiano mwingine wa siri. Mapenzi kati yao yalizaliwa muda mrefu sana. Lakini jambo jema ni kwamba wakati wa kazi ilikuwa kazi na wakati wa mapenzi ilikuwa mapenzi motomoto. Ofisi nzima walijua hilo, walichokuwa wakisubiri ni kuambiwa tu kama ndoa itakuwa kanisani au bomani.

"Tunaanzia wapi?" Gina akauliza.

"Nitakujuza ifikapo saa mbili usiku, kwa sasa tuachane na hili na tupange mipango mingine," Amata akamwambia.

✠ ✠ ✠

Madam S aliteremsha kioo cha gari alilokuwa akiliendesha. Kamanda Amata alikuwa hapo pembeni tayari kuzungumza na mwanamama huyo.

"Vipi. Mambo yanaenda?" akamuuliza.

“Ndiyo… ila kesho ikiwezekana tuonane ofisini asubuhi, najua nitakuwa na majibu mengi ya kukupa na hapo ndipo tutakuwa na picha ya kujua la kufanya,” Amata akamwambia Madam S.

“Sawa, saa nne kamili asubuhi kesho tukutane Shamba,” Madam S akamwambia Amata huku kile kioo kikipanda taratibu na lile gari kuondoka. Tayari ilitimu saa moja na nusu usiku, Amata na Gina walikuwa kwenye mgahawa wa Cucina Italiana kando ya barabara ya kuelekea Sea View Upanga. Mata baada ya kuongea na Madam S alirudi katika mgahawa ule na kumkuta Gina akiendelea na sharubati yake ya tende. “Kuna kazi Kunduchi Mtongani Beach Resort usiku wa leo… pia kuna kaziya kulisaka gari gari na kumpata mmiliki wake…” akamweleza Gina.

“Gari gani?” Gina akauliza.

“Mazda lililomgomga Madam S, muhimu ni kumpata dereva wake. Mpaka dakika hii linaonekana lipo Magomeni…” Amata akamwambia Gina.

“Ulitiwekea tracker?”

“Ndiyo!”

“Kwahiyo kazi yote hiyo uliifanya kwa muda mfupi tu?” Gina akazidi kudadisi.

“Yes sir!” Amata akajibu na wote wakacheka, “Umetembea na bastola?” akamuuliza.

“Nipo kamili boss, na mikono yangu inawasha sana maana siku hizi tumekaa tunanenepa tu hakuna misukosuko,” Gina akajibu na kuongeza hata yale ambayo hakutakiwa.

“Haya mama inatosha,” Amata akamkatisha huku akinyanyuka, “Twende Magomeni,” akamwambia.

“Jamani, si umesema saa nne?” Gina akauliza kwa mshangao huku nay eye akiinuka.
“We twende tukafanye kazi,” Amata akamamwambia. Wawili wale wakateremka ngazi mpaka chini ya lile jengo lililobeba mgahawa ule ndani yake. Wakaingia garini, Gina akiketi nyuma ya usukani na Amata katika siti ya abiria.
“Magomeni Kagera!” Amata akamwambia Gina na lile gari likaingia barabara ya Ocean Road kuifuata ile ya Ally Hassan Mwinyi. Dakika arobaini na tano tayari waliwakuwa mitaa ya Magomeni. Gina akaiacha Barabara ya Kawawa na kuchukua ile ya Morogoro kuitafuta Magomeni Kagera. Amata alikuwa akimwelekeza tu wapi pa kupita kadiri ya simu yake ilivyokuwa ikimwonesha.
Kagera Bar Lounge, ndipo lile gari lilipokuwa limeegeshwa. Gina akatafuta mahala pazuri ambapo isingemsumbua kutoka kama ingehitajika kufanya hivyo kwa haraka. Wakabaki ndani kwanza.
“Tunafanyaje? Tunamvamia ndani au tunasubiri hapa mpaka atoke?” Gina akauliza.
“Gina, mbona una maswali sana leo vipi?” Amata akauliza.
“Nna hamu ya kazi…”
“Sawa, nenda ndani ya hiyo bar hakikisha unamnasa, nakupa nusu saa tu…” Amata akamwambia.
“Sasa nitamjuaje?” Gina akahoji kwa utulivu.
“Nenda, mwambia DJ atangaze kuwa mwenye gari aina ya Mazda Jeusi mtajie na namba anahitajika nje, atatoka utamuona!” Amata akatoa maelekezo.
“Kazi ndogo sana!”

Nini Gina atafanya? Je kitendawili hicho kitateguka usiku huo?


Tuandikie Whatsapp

**0766974865**

Riwaya hii itapatikana kwa Tsh **5500** kuanzia tarehe 20/1/2026